

Asante kwa kutuchagua tushughulikie mahitaji yako ya afya. Lengo letu ni kuwapa wagonjwa wote huduma za juu za afya licha ya hali zao za kifedha. Tunatoa usaidizi wa kifedha kwa wagonjwa kwa huduma za dharura na nyingine za afya kwa mujibu wa Sera yetu ya Usaidizi wa Kifedha (Sera).

### Ni Nani Anastahiki?

Tunatoa usaidizi wa kifedha kwa wagonjwa wanaotimiza masharti ya Sera yetu. Ustahiki unalingana na vigezo vingi, ikiwa ni pamoja na bima na vyanzo vingine vya malipo (kama vile kwa ajili ya madai ya majeraha ya kibinafsi), mapato, ukubwa wa familia na mali. Sera hii inatoa huduma isiyolipishwa kwa wale ambao wamejaribu aina nyingine zote za malipo, na:

- Wana mapato ya familia yasiyozidi 250% ya mwaka huu kwa mujibu wa Mwongozo wa Serikali kuhusu Umaskini;
- Wametuma ombi ambalo limekamilishwa ipasavyo.

Iwapo umetimiza masharti ya kupata usaidizi wa kifedha, hutatozwa zaidi ya kiasi cha jumla cha huduma za dharura au za matibabu.

Usaidizi wa kifedha kwa walio na matumizi ya juu ya matibabu unaweza pia kupatikana iwapo umekumbwa na tukio kubwa la matibabu na linalohitaji fedha nyingi.

### Mahali pa Kupata Nakala Zisizolipishwa za Sera na Fomu za Ombi la Usaidizi wa Kifedha

Nakala zetu za Sera na Fomu za Ombi zinapatikana bila malipo kwa kuwasiliana nasi kwa kutumia maelezo yaliyoorodheshwa upande wa kulia. Unaweza kuomba nakala hizi kupitia simu, posta, au barua pepe. Zinaweza kupakuliwa na kuchapishwa kutoka kwenye tovuti zetu. Nakala hizi pia zinapatikana katika maeneo yetu yote ya hospitali kwenye madawati ya maelezo, afisi za usajili au idara za masuala ya dharura.

### Tafsiri Zinapatikana

Tafsiri za Sera yetu, Fomu za Ombi na Muhtasari huu zinapatikana katika lugha nyingine ukiomba au ukitembelea tovuti zilizoorodheshwa upande wa kulia.

### Usaidizi Unapatikana

Washauri wa Masuala ya Kifedha na Manufaa wanapatikana ili kukusaidia kukamilisha ombi lako la usaidizi wa kifedha. Unaweza kuwafikia kwa kupiga simu au kuwasiliana nao kama ilivyofafanuliwa katika sehemu ya "Jinsi ya Kutuma Ombi". Wanaweza pia kukusaidia ujisajili kwenye bima kupitia mipango ya Health Insurance Exchange au State of Michigan Medicaid.

### Jinsi ya Kutuma Ombi

#### Beaumont Health

- Ana kwa ana katika Hospitali yoyote ya Beaumont, ikiwa ni pamoja na tawi lililo katika 3601 W. 13 Mile Rd., Royal Oak, MI 48073
- Kupitia barua, andika kwa Usaidizi wa Kifedha Beaumont Health, 3601 W. 13 Mile Rd., Royal Oak, MI 48073
- Kwa kupiga simu kwa 877.687.7309
- Kwa kwenda kwenye [beaumont.org/patients-families/billing/financial-assistance](https://www.beaumont.org/patients-families/billing/financial-assistance)
- Kwa kutuma barua pepe kwa [EastFinancialCounseling@corewellhealth.org](mailto:EastFinancialCounseling@corewellhealth.org)

#### Spectrum Health Lakeland

- Ana kwa ana katika Hospitali yoyote ya Spectrum Health Lakeland, ikiwemo katika hospitali kuu iliyoko 1234 Napier Avenue, St. Joseph, MI 49085
- Kupitia barua, andika kwa Ushauri wa Kifedha wa Spectrum Health Lakeland, 1234 Napier Avenue, St. Joseph, MI 49085
- Kwa kupiga simu kwa 844.408.4103
- Kwa kutembelea [spectrumhealthlakeland.org/patient-visitor-guide/patient/billing/financial-assistance](https://www.spectrumhealthlakeland.org/patient-visitor-guide/patient/billing/financial-assistance)
- Kwa kutuma barua pepe kwa [SHLFinancialCounseling@spectrumhealth.org](mailto:SHLFinancialCounseling@spectrumhealth.org)

#### Spectrum Health

- Ana kwa ana kwa Hospitali yoyote ya Spectrum Health, ikiwa ni pamoja na hospitali kuu inayopatikana 100 Michigan, Grand Rapids, MI 49503
- Kupitia barua, andika kwa Ushauri wa Kifedha wa Spectrum Health, 100 Michigan, Grand Rapids, MI 49503
- Kwa kupiga simu kwa 844.838.3115
- Kwa kutembelea [spectrumhealth.org/billing/financial-assistance](https://www.spectrumhealth.org/billing/financial-assistance)
- Kwa kutuma barua pepe kwa [FinancialCounseling@spectrumhealth.org](mailto:FinancialCounseling@spectrumhealth.org)